

TANGAZO LA KAZI

1.0 KUHUSU ELCT ND SACCOS

ELCT ND SACCOS LTD ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichoanzishwa mwaka 1994 na kusajiliwa tarehe 27.07.1995 kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vyta Ushirika namba 15 ya mwaka 1991 kwa jina la ELCT- ND Savings and Credit Cooperative Society LTD na nambari ya usajili PRI-KJR-MSH-MC-2022-477. Makao makuu ya ELCT ND SACCOS yapo Mkoa wa Kilimanjaro – Moshi Mjiini ikiwa na Matawi yafuatayo:- Moshi, Himo, Mwika, Hai, Arusha, Karatu na Tabora inayohudumia Wanachama zaidi ya elfu kumi na tano (15,000) Nchini Tanzania.

2.0 NAFASI YA KAZI

ELCT ND SACCOS inatangaza nafasi (135) ya kazi ya muda (Mkataba wa miezi mitatu/sita) ya "**Afisa wa Mauzo**" mwenye uwezo, ubunifu, ujuzi na uzoefu katika sekta ya Vyama vyta Ushirika wa kifedha hasa SACCOS, ili kusaidia kufanya mauzo na kutangaza huduma na bidhaa za ELCT ND SACCOS katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia fungamano la pamoja kama ilivyo kwenye Masharti. Afisa Mauzo atawajibika katika Idara ya Masoko na atakuwa analipwa kwa "**KAMISHENI**" kulingana na makubaliano ya Mkataba.

3.0 MAJUKUMU YA AFISA MAUZO

Afisa Mauzo atakuwa na majukumu yafuatayo:

- i. Kufikia au kuzidi malengo ya mauzo ya kila wiki na mwezi
- ii. Kuvinjari na kutembelea maeneo uliyopewa ili kuwasilisha huduma na bidhaa za ELCT ND SACCOS kwa Wateja watarajiwa.

- iii. Kusaidia usimamizi katika kutambua mikakati inayofaa ya uuzaaji na bei za huduma na bidhaa za ELCT ND SACCOS.
- iv. Kuonyesha sifa za huduma na bidhaa kwa Wanachama na wasio Wanachama.
- v. Kuwasiliana na Viongozi na kuweka miadi ya kuwasilisha bidhaa za ELCT ND SACCOS.
- vi. Kuhudhuria maonyesho ya biashara na hafla zingine zinazohusiana na tasnia ya uuzaaji wa huduma na bidhaa za ELCT ND SACCOS.
- vii. Kuandaa mapendekezo ya mauzo kwa Wanachama watarajiwa.
- viii. Kukamilisha ripoti za mauzo za kawaida zinazobainisha idadi ya mauzo yaliyofanywa.
- ix. Kuhakikisha Wanachama wote waliojisajili na ELCT ND SACCOS wanatumia huduma na bidhaa za Chama.
- x. Kutoa elimu ya huduma na bidhaa za ELCT ND SACCOS kwa wadau mbalimbali hasa maeneo yenye shughuli za kiuchumi.
- xi. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake.

4.0 SIFA NA UJUZI

- a. Awe na umri kuanzia miaka 18 na zaidi
- b. Awe ni Mtanzania;
- c. Awe na Elimu angalau kuanzia Astashahada (Certificate) na kuendelea
- d. Awe na uzoefu katika kufanya masoko usiopungua mwaka mmoja (1)
- e. Awe na uwezo wa kujisimamia mwenyewe
- f. Awe na ubunifu na ujuzi wa kutekeleza ubunifu wake katika mambo yote yanayohusu uuzaaji wa bidhaa na huduma za ELCT ND SACCOS.
- g. Awe na ujuzi wa matumizi ya mifumo na vifaa vyta kompyuta
- h. Mwenye ufahamu wa Utawala wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa kuzingatia Sheria ya Ushirika ya mwaka 2013 atapewa kipaumbele.

5.0 VIAMBATISHO

- a. Alete Barua ya maombi ya kazi
- b. Aambatishe Wasifu Binafsi (CV)
- c. Aweke Nakala ya Vyeti vya masomo na cheti cha kuzaliwa vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Mahakama
- d. Alete picha mbili (2) za "passport size" za sasa
- e. Nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- f. Barua za wadhamini wawili (2), na angalau mmoja anakufahamu katika utendaji kazi wako

6.0 MAELEKEZO MENGINE

- a. Mwombaji aonyeshe mawasiliano yake bayana
- b. Mwombaji atakayekuwa amekidhi vigezo na sifa tajwa ataarifiwa kwa ajili ya taratibu zingine zinazofuata.
- c. Kama mwombaji hataatarifiwa cho chote kuhusu maombi yake kwa kipindi cha siku thelathini (30) tangu kipindi cha mwisho wa tarehe ya mwisho ya maombi atajihesabia kuwa hajafanikiwa.

7.0 JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua za maombi zielekezwe kwa;

**MENEJA MKUU,
ELCT ND SACCOS,
S.L.P 7779 MOSHI.**

Barua za maombi ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kuwasilishwa kupitia barua pepe ya masoko@elctndssaccos.org kabla ya tarehe 11 Februari 2024 saa 06:00 Usiku.

Imetolewa leo tarehe 20-01-2023 na MENEJA MKUU WA ELCT ND SACCOS

